



## TAARIFA KWA UMMA

### UTOAJI WA HUDUMA ZA MAWASILIANO BILA LESENI

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) inapenda kuutaarifu Umma kuwa utoaji wa huduma za mawasiliano, zikiwemo huduma za usalama mtandaoni (cybersecurity services), intaneti, na vituo vya kutunzia data (data centres), katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuwa na leseni iliyotolewa na TCRA ni kinyume na Kifungu cha 14 cha Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2010 (EPOCA) ambacho kinakataza mtu, taasisi au kampuni yoyote kutoa huduma hizo bila kuwa na leseni.

Aidha, tunapenda kuukumbusha Umma kuepuka kutumia huduma za mawasiliano, zikiwemo huduma za usalama mtandaoni, intaneti, na vituo vya kutunzia data, zinazotolewa na mtu, taasisi au kampuni zisizo na leseni zilizotolewa na TCRA.

TCRA inaendelea kusimamia huduma za mawasiliano nchini na haitasita kuchukua hatua kisheria dhidi ya mtu, taasisi au kampuni itakayobainika kujihusisha na utoaji wa huduma za mawasiliano, zikiwemo huduma za usalama mtandaoni, intaneti na vituo vya kutunzia data, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania bila kuwa na leseni iliyotolewa na TCRA

Kwa taarifa zaidi wasiliana nasi kupitia nambari 0800 008 272 au baruapepe: [dawatilahuduma@tcra.go.tz](mailto:dawatilahuduma@tcra.go.tz).

Imetolewa tarehe **18 Januari 2024.**

Dkt. Jabiri K. Bakari  
**MKURUGENZI MKUU**